# JUNIOR SECONDARY SCHOOL ASSESSMENT
# MONITORING LEARNER'S PROGRESS
# GREDI YA NANE – 004
# KISWAHILI LUGHA – KARATASI YA 1

Jina ____________________________________________

Jinsia Mvulana ☐ Msichana ☐

Jina la Shule ____________________________________

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**

Vifaa vya kidijitali vimeleta mapinduzi makubwa katika maisha ya binadamu hasa katika Nyanja za mawasiliano, elimu, biashara na burudani. Simu janja, kompyuta na vidubini vingine vimewezesha watu kuwasiliana kwa haraka kupitia mitandao ya kijamii kama vile WhatsApp na Facebook. Kwa upande wa elimu, wanafunzi wanapata rasilimali mbalimbali mtandaoni, jambo linalorahisisha ujifunzaji na kuongeza ufanisi katika tafiti.

Katika sekta ya biashara, matumizi ya vifaa vya kidijitali yamerahisisha ununuzi na uuzaji wa bidhaa kupitia majukwaa kama Jumia na Amazon. Kuna watu wanaotumia vifaa hivi kufanya kazi za mtandaoni kama uandishi wa maudhui na uchambuzi wa data. Hali hii imeleta fursa mpya za ajira na kuongeza kipato kwa watu wengi duniani.

Hata hivyo, matumizi ya vifaa vya kidigitali yanahitaji tahadhari kubwa. Kutegemea vifaa hivi kupita kiasi kunaweza kusababisha uraibu, kupunguza umakini n ahata kuathiri afya ya macho kutokana na mwanga wa skrini. Watoto na vijana wanapaswa kupewa mwongozo mzuri kuhusu matumizi sahidi ya teknolojia ili kuepukana na madhara yanayoweza kujitokeza.

Kwa kuzingatia yote hayo, ni muhimu kutumia vifaa vya kidigitali kwa busara. Watu wanapaswa kuweka mipaka katika matumizi ya vifaa hivi ili kuwa na maisha yenye uwiano kati ya teknolojia na shughuli za kijamii. Pia, elimu juu ya usalama wa mtandaoni ni muhimu ili kuepuka madhara kama udukuzi na utapeli wa mtandaoni.

1. Ni ipi kati ya hizi ni faida ya matumizi ya vifaa vya kidijitali?
   A. Kupunguza mawasiliano duniani B. Kurahisisha upatikanaji wa elimu
   C. Kuharibu afya ya macho D. Kupunguza nafasi ya ajira
2. Vifaa vya kidijitali vimetumiwa zaidi kwa shughuli zipi?
   A. Kilimo na uvuvi B. ufugaji C. mawasiliano, biashara na elimu D. udukuzi
3. Ni madhara yapi yanayoweza kusababishwa na matumizi ya kupita kiasi ya vifaa vya kidijitali?
   A. Kuongeza umakini B. kuleta uraibu
   C. kuimarisha afya ya macho D. kuongeza maarifa
4. Kwa nini ni muhimu kuwa na elimu ya usalama wa mitandaoni?
   A. Ili kutumia mitandao bila kipimo B. kuepuka udukuzi na utapeli
   C. kuzidisha maarifa ya kuwatapeli watu D. ili kuwazuia wengine kutotumia mitandao
5. Zifuatazo ni mbinu sahihi za kuhakikisha matumizi bora ya vifaa vya kidijitali ila?
   A. Kutumia nywila Imara na kuepuka kushiriki taarifa binafsi
   B. Kuweka mipaka ya muda wa kutumia vifaa hivyo
   C. Kuzingatia usalama wa mtandaoni na kuepuka tovuti hatarishi
   D. Kuwasiliana na watu usiowajua mitandaoni
6. Ni nini maana ya uraibu kulingana na kifungu hiki?
   A. Kutumia kwa kiasi vifaa vya kidijiatali
   B. kutumia na kutegemea kupita kiasi vifaa vya kidijitali
   C. kufurahia vifaa vya kidijitali D. kupunguza matumizi ya vifaa

**Soma kifungu kifuatacho kisha uyajibu maswali**

Katika milima ya Kisiwa cha Madoa, aliishi kenge mweusi mwenye jina la kipekee: Kenge wa Giza. Kenge huyu hakupenda msongamano wala kelele, hivyo akaamua kuishi peke yake kwenye kivuli cha mawe makubwa. Aliwaupeka viumbe wengine, lakini alikuwa na uwezo wa pekee wa kujificha kwa ustadi mkubwa kiasi kwamba hata mnyama aliyekuwa karibu hangeweza kumwona.

C. Kutabiri matukio ya siku za baadaye D. Kuwa mganga mahiri baina ya watu wa jamii yake.

13. Hadithi hii ni ya aina gani?
A. Visakale B. mighani C. hurafa D. hekaya

14. Syokimau alitabiri matukio yafuatayo isipokuwa
A. Kuzuka kwa ndwele zisizo na tiba B. Kuzuka kwa kizazi ambacho kitavunja miko
C. Uvamazi wa jamii yake na jamii jirani D. Joka lililotema moto pamoja na moshi

15. Nguvu za kiajabuajabu alizokuwa nazo Syokimau ni zifuatazo ila
A. Kufa na kufufuka mara mbili kabla yake kufa kabisa
B. Kutabiri mambo na mwishowe yakatimia
C. Kushirikiana na wazungu kujenga reli
D. Kuugua ndwele zilizowasumbua watu wa jamii yake na kupona

16. Watu waliokuwa na nguvu za kiajabuajabu kutoka jamii mbalimbali walijulikana kama
A. Majagina B. viongozi C. waheshimiwa D. walanguzi

17. Ni tukio lipi linafanya jina la Syokimau kukumbukwa na kizazi cha sasa?
A. Kufa na kufufuka mara mbili B. Jina lake kuitanishwa na mji fulani
C. Kuzaliwa miaka ya zamani D. Kuugua maradhi ya kishirikina

18. Ni kauli ipi ya kweli kulingana na kifungu hiki
A. Jamii ya Akamba ilijenga reli
B. Uhasama baina ya Akamba na jamii jirani ulisababisha mavamizi
C. Mnara umejengwa katika kituo cha reli cha Syokimau kwa heshima ya Akamba
D. Makao ya Syokimau yalikuwa karibu na kituo cha reli

**Tumia jedwali lifuatalo kujibu maswali yafuatayo**

| Siku | Salama | Juma | Kigeni | Bahati |
|---|---|---|---|---|
| Jumatatu | Machungwa | Ndizi | Parachichi | Nyanya |
| Jumanne | Parachichi | Nyanya | Machungwa | Ndizi |
| Jumatano | Ndizi | Parachichi | Nyanya | Machungwa |
| Alhamisi | Nyanya | Machungwa | Ndizi | Parachichi |
| Ijumaa | Machungwa | Nyanya | Parachichi | Ndizi |

19. Ni mteja yupi anayenunua nyanya mara nyingi zaidi kwa wiki?
A. Salama B. Kigeni C. Bahati D. Juma

20. Ni kauli ipi ya kweli kati zifuatazo kuhusu bidhaaa zilizonunuliwa siku ya Ijumaa?
A. Wateja wote walinunua matundaB. wateja wawili walinunua nyanya
C. kila mteja alinunua bidhaa tofauti D. Bahati hakununua kitu chochote

**Jaliza nafasi zilizo wazi katika kifungu kifuatacho**

Elimu _____21______ ufunguo wa maisha. _______22_______ mtu asiyeelimika hupatwa na changamoto nyingi maishani. Kwa hivyo ni wajibu wetu ________23_________ maarifa bora katika kila hatua ya masomo________24_______ Tutapata mafanikio iwapo tutajitahidi. Ni sharti ______25_______ bidii na nidhamu tunaposoma. Wanafunzi wanapaswa pia kuheshimu walimu _______26________. Ni ________27_______ kuhudhuria vipindi __________28__________ kwa wakati unaofaa. ________29___________ jamii inapaswa kuunga mkono juhudi za kielimu kwa kuwa ________30______.

21. A. ni B. si C. bora D. ingawa
22. A. basi B. hata hivyo C. ikiwa D. bila shaka
23. A. kuchezea maarifa B. kujipatia C. kushangilia D. kushabikia
24. A. ; B. . C.: D. /
25. A. tuonyeshe B. tuangamize C. tupuuze D. tuhepe
26. A. wanapotufundisha B. wanapokosolewa C. wanapowasifu D.wanapowashauri
27. A. ajabu B. vyema C. nadra D. hiari
28. A. vizuri B. vichache C. vyote D. vyovyote
29. A. kila B. baadhi ya C. sote D. wote
30. A. mtoto akililia wembe mpe B. elimu ni taa gizani huzagaa
C. samaki mkunje angali mbichi D. subira huvuta heri

**Kutoka swali la 31 jibu kulingana na maagizo ya swali**

31. Maneno **mchanga, chumvi, sukari** hupatikana katika ngeli ipi?
A. I-ZI B. U-U C. U-YA D. I-I

32. Ni kauli ipi yenye amri kati ya hizi
A. Ondokeni hapa! B. Wakisoma watafuzu. C. Waliambiwa warudi darasani

33. Ni sentensi ipi iliyotumia kivumishi cha **a-unganifu** cha kuonyesha aina
A. Gari la mwalimu limefika B. Kalamu ya kuandikia imenunuliwa
C. Jumba la mawe limebomolewa D. Wangesoma wangefuzu

34. Andika katika wingi: **Mkunga alivuliwa kutoka baharini.**
A. Wakunga walivuliwa kutoka mabaharini B. Mikunga zilivuliwa kutoka baharini
C. Mikunga walivuliwa kutoka baharini D. Kiatu cha mwanafunzi kimepotea

35. Ni nini ukanusho wa: **Utamwona utakapofika.**
A. Hautamwona utakapofika B. Hutamwona usipofika
C. Utamwona usipofika D. Usimwone utakapofika

36. Ni orodha gani iliyo na **viwakilishi pekee?**
A. Njoo, ongea, keti, amua B. mimi, sisi, nyinyi, Baraka
C. shuleni, nchini, nyumbani D. yule, gani, chake, wangu

37. Chagua sentensi yenye **kivumishi halisi**
A. Mtoto mwingine amepokea tuzo B. Vazi la Bi. Harusi lilikuwa lakupendeza
C. Vikapu vivyo hivyo vimeletwa na wageni D. Mtoto yupi amedhulimiwa?

38. Ni sentensi ipi kati ya hizi iliyo katika **kauli ya kutendewa**
A. Mama alioshewa nguo zake na shangazi Kanze
B. Mwalimu alishangazwa na utundu wa mwanafunzi
C. Wageni walitembezwa kote mbugani
D. Mtoto alioshwa kwa wakati ufaao

39. Nomino ipi kati ya hizi inapatikana katika ngeli ya **U-ZI**
A. Waya B. ugonjwa C. ugali D. chumvi

40. "Yeye ni mchwa kazini" ina maana kuwa
A. Ana bidii kazini B. anafanana na mchwa C. anapenda mchwa. D. ni mdogo kama mchwa

41. Chagua neno linaloonyesha kinyume cha: Chache
A. Bora B. nyingi C. fupi D. dogo

42. Chagua nomino dhahania kutoka kwenye orodha ifuatayo:
A. Meza B. kalamu C. uyoga D.furaha

43. Chagua sentensi iliyo na kitenzi kishirikishi
A. Anaendelea kusoma B. Atasoma kwa bidii C. Atasoma kesho D. wamekuwa wakisoma

44. Chagua neno lililo katika ngeli ya LI-YA
A. Ua B. ukuta C. ugonjwa D. ufagio

45. Sentensi ipi ni **sahili?**
A. Mchezo wa soka umechezwa uwanjani B. Alifika ila hakumwona
C. Magari ambayo yalioshwa yalibeba wageni D. Tutashiriki karamu iwapo tutaalikwa

46. Jaza kwa kiambishi ngeli bora zaidi: Bustani ___tafagiliwa.
A. Ya B. u C. li D. I

47. Kamilisha kitendawili kifuatacho: Popote niendapo hunifuata ______________
A. Upepo B. mwangaza C. rafiki D. kivuli

48. Ni kipi kielezi cha namna kati ya sentensi zifuatazo?
A. Jana tulichelewa shuleni B. watoto walicheza kwa makini
C. alifika usiku D. alifunza mara kwa mara

49. Ni sentensi ipi inaonyesha hali ya mazoea?
A. Wakulima wengi wangali wanalima mashambani
B. Watalii kadhaa husafiri wakati wa kiangazi
C. Mitandao imevumbuliwa hivi majuzi
D. Wanafunzi wangesoma kwa bidii wangefaulu

50. Kamilisha methali ifuatayo: Mchumia juani
A. Hula na wakwao B. hunywa maji maenge C. huchoka sana D. hulia kivulini

**Kutoka swali la 31 jibu kulingana na maagizo ya swali**

31. Maneno **mchanga, chumvi, sukari** hupatikana katika ngeli ipi?
A. I-ZI B. U-U C. U-YA D. I-I

32. Ni kauli ipi yenye amri kati ya hizi
A. Ondokeni hapa! B. Wakisoma watafuzu. C. Waliambiwa warudi darasani

33. Ni sentensi ipi iliyotumia kivumishi cha a-**unganifu** cha kuonyesha aina
A. Gari la mwalimu limefika B. Kalamu ya kuandikia imenunuliwa
C. Jumba la mawe limebomolewa D. Wangesoma wangefuzu

34. Andika katika wingi: **Mkunga alivuliwa kutoka baharini.**
A. Wakunga walivuliwa kutoka mabaharini B. Mikunga zilivuliwa kutoka baharini
C. Mikunga walivuliwa kutoka baharini D. Kiatu cha mwanafunzi kimepotea

35. Ni nini ukanusho wa: **Utamwona utakapofika.**
A. Hautamwona utakapofika B. Hutamwona usipofika
C. Utamwona usipofika D. Usimwone utakapofika

36. Ni orodha gani iliyo na **viwakilishi pekee?**
A. Njoo, ongea, keti, amua B. mimi, sisi, nyinyi, Baraka
C. shuleni, nchini, nyumbani D. yule, gani, chake, wangu

37. Chagua sentensi yenye **kivumishi halisi**
A. Mtoto mwingine amepokea tuzo B. Vazi la Bi. Harusi lilikuwa lakupendeza
C. Vikapu vivyo hivyo vimeletwa na wageni D. Mtoto yupi amedhulimiwa?

38. Ni sentensi ipi kati ya hizi iliyo katika **kauli ya kutendewa**
A. Mama alioshewa nguo zake na shangazi Kanze
B. Mwalimu alishangazwa na utundu wa mwanafunzi
C. Wageni walitembezwa kote mbugani
D. Mtoto alioshwa kwa wakati ufaao

39. Nomino ipi kati ya hizi inapatikana katika ngeli ya **U-ZI**
A. Waya B. ugonjwa C. ugali D. chumvi

40. **"Yeye ni mchwa kazini"** ina maana kuwa
A. Ana bidii kazini B. anafanana na mchwa C. anapenda mchwa D. ni mdogo kama mchwa

41. Chagua neno linaloonyesha kinyume cha: Chache
A. Bora B. nyingi C. fupi D. dogo

42. Chagua nomino dhahania kutoka kwenye orodha ifuatayo:
A. Meza B. kalamu C. uyoga D.furaha

43. Chagua sentensi iliyo na kitenzi kishirikishi
A. Anaendelea kusoma B. Atasoma kwa bidii C. Atasoma kesho D. wamekuwa wakisoma

44. Chagua neno lililo katika ngeli ya LI-YA
A. Ua B. ukuta C. ugonjwa D. ufagio

45. Sentensi ipi ni **sahili?**
A. Mchezo wa soka umechezwa uwanjani B. Alifika ila hakumwona
C. Magari ambayo yalioshwa yalibeba wageni D. Tutashiriki karamu iwapo tutaalikwa

46. Jaza kwa kiambishi ngeli bora zaidi: Bustani ___tafagiliwa.
A. Ya B. u C. li D. I

47. Kamilisha kitendawili kifuatacho: Popote niendapo hunifuata ______________
A. Upepo B. mwangaza C. rafiki D. kivuli

48. Ni kipi kielezi cha namna kati ya sentensi zifuatazo?
A. Jana tulichelewa shuleni B. watoto walicheza kwa makini
C. alifika usiku D. alifunza mara kwa mara

49. Ni sentensi ipi inaonyesha hali ya mazoea?
A. Wakulima wengi wangali wanalima mashambani
B. Watalii kadhaa husafiri wakati wa kiangazi
C. Mitandao imevumbuliwa hivi majuzi
D. Wanafunzi wangesoma kwa bidii wangefaulu

50. Kamilisha methali ifuatayo: Mchumia juani
A. Hula na wakwao B. hunywa maji maenge C. huchoka sana D. hulia kivulini